**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 03 Mei 2004 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.

4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Taja faida nne za kutumia mbinu ya uigizaji katika somo la Kiswahili.
2. Eleza kwa mfano tofauti kati ya shairi na ngonjera katika Kiswahili.
3. Toa hoja nne za kuonyesha umuhimu wa nahau katika mawasiliano ya kila siku.
4. Bainisha mambo manne ya kuzingatia katika kusoma kwa sauti.
5. Eleza tofauti kati ya barua ya kikazi na barua ya kirafiki.
6. Taja hatua nne ambazo mwalimu hutumia kuandaa andalio la somo.
7. Eleza sifa nne zinazojitokeza kwa mwandishi bora wa barua ya magazetini.
8. Toa hoja nne kuthibitisha nafasi ya nyimbo za jadi katika kujenga mshikamano wa kijamii.
9. Bainisha aina nne za tungo katika Kiswahili na fafanua nafasi yake.
10. Eleza umuhimu wa shajara ya mwalimu katika maandalizi ya kazi za kila siku.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Jadili namna vitendawili vinavyoweza kutumika kama nyenzo ya kufundisha lugha.
12. Kwa hoja tano, eleza jinsi mbinu ya kazi za vikundi inavyoboresha fikra za wanafunzi.
13. Eleza hatua kuu nne za mchakato wa ufundishaji ukitoa mifano.
14. Kwa hoja tano, eleza nafasi ya Kiswahili katika kukuza mshikamano wa kitaifa.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza sifa tano za zana zinazofaa kutumika katika ufundishaji wa Kiswahili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

16. Jadili faida tano za kutoa majaribio ya mara kwa mara kwa wanafunzi.

17. Eleza mbinu tano ambazo mwalimu anaweza kutumia kufanikisha somo la insha.

18. Eleza changamoto tano zinazojitokeza wakati wa kutumia mbinu ya mihadhara darasani.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org